

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Kumb.Na. AC/34/325/72/72

23/08/2019

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale anawatangazia Waombaji wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi za Katibu Mahsusii III (nafasi 03) na Mtendaji wa Kijiji III (nafasi 04) kama ifuatavyo;

### 1. KATIBU MAHSUSII III (Nafasi - 03)

Ngazi ya Mshahara TGS B1 sawa na Tshs 390,000/= kwa mwezi.

#### SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa Wahitimu wa kidato cha IV waliohudhuria Mafunzo ya Uhaziri na kufauli Mtihani wa hatua ya tatu. Wawe wamefaulu somo la Hati mkato ya Kiswahili na Kiingereza Maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambulika na Serikali na kupata cheti katika Programu za **Windows, Microsoft Office, Internet, E-Mail na Publisher.**

#### KAZI NA MAJUKUMU YA KATIBU MAHSUSII III

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kusaidia kutunza taarifa / kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

## **2. MTENDAJI WA KIJIKI III (Nafasi - 04)**

Ngazi ya Mshahara TGS B1 sawa na Tshs 390,000/= kwa mwezi.

### **SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye elimu ya kidato cha IV au VI aliyehitimu mafunzo ya **Astahhada/ Cheti (Technician Certificate NTA - LEVEL 5)** katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii, na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### **KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI III**

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- II. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa amani na kusimamia Utawala bora katika Kijiji.
- III. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- IV. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- V. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria, na Taratibu.
- VI. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- VII. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.
- VIII. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- IX. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- X. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- XI. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- XII. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

### **MASHARTI KWA UJUMLA**

- a) Mwombaji awe ni Mtanzania asiezidi umri wa miaka 45, awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya Nyang'hwale.
- b) Mwombaji awe hajawai kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi wa Umma.
- c) Mwombaji aambatishe taarifa zake binafsi (CV) ikionyesha sanduku la posta, E-mail, namba za simu anazotumia na uzoefu wake kazini.

- d) Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya Taaluma, cheti cha kidato cha IV au VI, cheti cha kuzaliwa na picha mbili (2) (passport size) za hivi karibuni.
- e) Mwombaji anatakiwa aambatanishe vyeti vilivyo **sainiwa na kupigwa muhuli (CERTIFIED COPY)** na Mwanasheria au Mahakama.
- f) Mwisho wa kupokea barua za maombi ni terehe **06/09/2019** siku ya Ijumaa saa 09:30 **Alasiri**. Maombi yote yawasilishwe kwa Anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,

HALMASHAURI YA WILAYA,

S.L.P 352,

NYANG'HWALE.

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri [www.nyanghwaledc.go.tz](http://www.nyanghwaledc.go.tz)

  
Lucy D. Lyaruu

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

HALMASHAURI YA WILAYA

NYANG'HWALE

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR  
NYANG'HWALE DISTRICT COUNCIL  
P. O. BOX 352.  
GEITA

**Nakala:** Wakurugenzi Watendaji;

Halmashauri za Wilaya

**Bukombe, Chato, Geita**

**na Mbogwe.**

- Tafadhali Tangazo hili libandikwa  
katika mbao za matangazo.

Mkurugenzi wa Mji,

Halmashauri ya Mji,

**Geita.**

- Tafadhali Tangazo hili libandikwa  
katika mbao za matangazo.